TMDA
Tanzania Medicines & Medical Devices Authority

# KANDA YA ZIWA MASHARIKI
## Jarida la Mtandaoni



*Afisa wa TMDA akipokea kikombe na cheti kutoka kwa Mkuu wa Wilaya ya Nyamagana, Bi. Amina Makilagi wakati wa Maonesho ya Afrika Mashariki yaliyofanyika jijini Mwanza. TMDA iliibuka mshindi katika maonesho hayo kwa kundi la Taasisi za Serikali kuu na Serikali za mitaa.*

# TMDA YAIBUKA MSHINDI
## WA KWANZA MAONESHO YA BIASHARA AFRIKA MASHARIKI

Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) imeibuka mshindi wa kwanza Katika Kundi la Taasisi za Serikali Kuu na Serikali za Mitaa katika maonesho ya Biashara ya Afrika Mashariki katika Viwanja vya Rocky City Mall jijini Mwanza mwezi Septemba 2021.

TMDA ilishiriki katika maonesho hayo kwa lengo la kutoa elimu juu ya udhibiti wa ubora, usalama na ufanisi wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi pamoja na udhibiti wa bidhaa za tumbaku.

Katika maonesho haya hamasa kubwa iliwekwa katika umuhimu wa kutoa taarifa za madhara yanayohisiwa kusababishwa na matumizi ya dawa na vifaa tiba na athari za kiafya zinazo weza kusababishwa na matumizi ya bidhaa za tumbaku.

Mgeni rasmi katika hafla hiyo alikuwa Mkuu wa Mkoa wa Mwanza **Mhandisi Robert Gabriel** aliyewakilishwa na Mkuu wa Wilaya ya Nyamagana **Bi. Amina Magilagi**.

> ***Dhima yetu ni kulinda afya ya jamii kwa kuzuia athari zinazoweza kujitokeza kutokana na matumizi ya dawa, vitendanishi na vifaa tiba.***

# TMDA YATOA MAFUNZO MAALUMU YA DAWA TIBA ZENYE MADHARA YA KULEVYA



*Mganga Mkuu wa Mkoa wa Mwanza Dkt. Thomas Rutachunzibwa (kushoto) akizungumza na wataalamu wa afya walioshiriki katika mafunzo yaliyoandaliwa na TMDA Mwezi Oktoba, 2021.*

Watumishi wa sekta ya afya kutoka hospitali na Vituo vya Afya jijini Mwanza wamepewa mafunzo juu ya kuhifadhi na kusimamia matumizi ya dawa tiba zenye madhara ya kulevya, (Narcotics and Psychotropic drugs).

Mafunzo hayo yaliyohusisha Waganga Wakuu wa hospitali na vituo vya afya pamoja na wafamasia yaliyotolewa na Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) Kanda ya Ziwa Mashariki yalilenga kuwajengea uwezo na weledi katika kusimamia na kutunza dawa tiba zenye madhara ya kulevya.

Kaimu Meneja Kanda ya Ziwa Mashariki, **Bi. Sophia Mziray** aliwataka washiriki wa mafunzo hayo kuzingatia taratibu na miongozo ya utunzaji na usimamizi wa matumizi ya dawa tiba zenye madhara ya kulevya katika maeneo yao ya kazi.

"Dawa za aina hii zinahitaji udhibiti madhubuti kuanzia zinapoingia nchini hadi zinapomfikia mtumiaji kwa vile zisipotumika ipasavyo zinaweza kusababisha madhara makubwa ya kiafya kutokana na uasili wake wa kulevya" alisema Mziray.

Alisema kuwa ukaguzi wa mara kwa mara unaofanywa na TMDA katika maeneo ya huduma za afya umebaini mapungufu katika eneo la utunzaji na uandaaji wa taarifa za matumizi wa dawa hizo, na ndiyo sababu ya kuandaa na kuendesha mafunzo hayo kwa watendaji hao wa Sekta ya Afya.

Mkaguzi wa Dawa kutoka TMDA Kanda ya Ziwa Mashariki, **Bw. Mtani Njengere** aliwataka watumishi wanaohusika na uhifadhi na utoaji wa dawa hizo kwa matumizi ya wagonjwa, kuandaa kwa usahihi na kuhifadhi vyema taarifa za matumizi ya dawa hizo kwa mujibu wa taratibu zilizopo.

Mmoja wa washiriki wa mafunzo hayo, **Dkt. Zitta Rugenge** kutoka Kituo cha Afya Igoma aliupongeza uongozi wa TMDA kwa kuandaa na kutoa mafunzo hayo huku akiomba yawe endelevu kwa kushirikisha watumishi wengi zaidi ili kuongeza ufanisi na weledi katika utunzaji na usimamizi wa matumizi ya dawa hizi.

# MAABARA ZAKUTWA NA VITENDANISHI VYA SERIKALI

Vitendo vya maabara binafsi kukutwa vikitumia vitendanishi ambavyo ni mali ya Serikali kinyume na sheria vimeendelea kubainika katika kaguzi zinazofanywa na Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA).

Hili imebainika baada ya TMDA Ofisi ya Kanda ya Ziwa Mashariki kufanya ukaguzi katika maabara binafsi 88 jijini Mwanza na Manispaa ya Ilemela mwezi julai 2021 ambapo maabara 16 zilikutwa na vitendanishi ambavyo ni mali ya Serikali.

Msimamizi wa Dawati la Udhibiti wa Vifaa Tiba na Vitendanishi, TMDA Kanda ya Ziwa Mashariki, **Bw. Mtani Njegere** amesema kuwa kitendo cha kukutwa na vitendanishi vya Serikali katika maabara binafsi ni kosa kisheria na hatua za kisheria zimechukuliwa.

"Vitendanishi vya serikali vilivyokutwa katika maabara kinyume na sheria viliorodheshwa kwenye fomu ya kukamatia (confiscation form) na kuondolewa katika maabara hizo na hatua stahiki za kisheria kuchukuliwa" alisema.

Vilevile, **Bw. Njegere** alieleza kuwa katika ukaguzi huo dawa ambazo hazikuwa zimesajiliwa na TMDA zilikutwa katika maabara binafsi na kuwa dawa hizo ziliondolewa pia kwa kuorodheshwa kwenye fomu ya kukamatia (confiscation form).



*Wakaguzi wa TMDA wakifanya ukaguzi katika moja ya maabara binafsi katika manispaa ya Ilemela mkoani Mwanza mwezi Septemba, 2021.*

Aidha **Bw. Njegere** alieleza kuwa katika ukaguzi huo walibaini uwepo wa maabara 16 ambazo hazikuwa na usajili na watoa huduma ambao hawakuwa na sifa pamoja na utunzaji usio faa wa vitendanishi.

> ***Vitendanishi ambavyo vinahitaji hali ya ubaridi vilikutwa havijahifadhiwa kwenye jokofu na ambavyo vimekwisha muda wake wa matumizi, pia vilibainika wakati wa ukaguzi***
>
> ***-Bw. Njegere***

Aliongeza kuwa walibaini uwepo wa maabara ambazo zimekuwa zikitoa huduma za kitabibu kama vile kuchoma sindano na kuuza dawa kinyume na utaratibu.

# HABARI PICHA




*Mganga Mkuu wa Mkoa wa Simiyu, **Dkt. Bonphace Marwa** akizungumza wakati wa kikao kazi na Viongozi wa Mkoa, Halmashauri na watendaji wa sekta ya afya na wafanyabiashara juu ya shughuli za udhibiti wa bidhaa za tumbaku mkoani Simiyu mwezi Novemba, 2021.*



*Meneja TMDA Ofisi ya Kanda ya Ziwa Mashariki **Bi. Sophia Mziray** akizungumza na Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mwanza, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi (SACP) Ramadhan Ngh'anzi, alipomtembelea ofisini kwake mwezi Septemba, 2021.*



*Wananchi wa Kijiji cha Mhungwe kata ya Mabuki Wilaya ya Misungwi wakihamasishwa juu ya umuhimu wa kuchanja chanjo ya UVIKO-19 ambapo wananchi 12 walihamasika na wakukubali kuchanja chanjo ya UVIKO-19 mwezi Oktoba, 2021.*



*Mkaguzi Msaidizi wa Dawa **Bw. Frank Mhini** akitoa elimu juu ya matumizi sahihi ya dawa za binadamu kwa wanafunzi wa shule ya sekondari ya J.K Nyerere katika Halmashauri ya Wilaya ya Tarime mkoani Mara mwezi Oktoba, 2021.*

# HABARI PICHA



*Mkaguzi wa Dawa, TMDA Kanda ya Ziwa Mashariki* ***Bw. Mtani Njegere*** *akitoa elimu juu ya matumizi sahihi ya dawa za binadamu kwa wanafunzi wa shule ya Sekondari Ngudu Wilayani Kwimba mwezi Oktoba, 2021.*




*Mkaguzi wa Dawa, Kanda ya Ziwa Mashariki* ***Bw. Aggrey Muhabuki*** *akiwasilisha mada wakati wa kikao kazi na viongozi wa Mkoa, Watendaji wa Halmashauri na wataalamu wa sekta ya Afya wa Mkoa wa Mwanza kuhusu udhibiti wa Bidhaa za Tumbaku nchini katika ukumbi wa mikutano wa TMDA jijini Mwanza mwezi Septemba, 2021.*




*Mkaguzi wa TMDA, Kanda ya Ziwa Mashariki* ***Bw. Aggrey Muhabuki*** *akifanya ukaguzi katika moja ya duka la dawa za binadamu wilayani Bunda, mkoa wa Mara mwezi Disemba, 2021.*




*Afisa wa TMDA, Kanda ya Ziwa Mashariki* ***Bw. Waridi Msumari*** *akimweleza Mkuu wa Wilaya ya Nyamagana,* ***Bi. Amina Makilagi*** *kazi na majukumu ya TMDA wakati wa Maonesho ya Afrika Mashariki yaliyofanyika katika viwanja vya Rock City Mall jijini Mwanza mwezi Septemba, 2021.*

# TMDA KANDA YA ZIWA MASHARIKI YAANZA UDHIBITI WA BIDHAA ZA TUMBAKU MKOANI MWANZA



*Katibu Tawala Wilaya ya Ilemela, **Said Kitinga** akizungumza wakati wa kikao kazi baina ya TMDA na viongozi wa Mkoa, Halmashauri na Watendaji wa Sekta ya Afya ya mkoa wa Mwanza kilichofanyika mwezi Septemba, 2021 katika Ukumbi wa TMDA Mwanza.*

Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) imetangaza mkakati (Action Plan) wa miaka mitatu kudhibiti matumizi holela ya bidhaa za tumbaku ili kuwakinga wasiovuta na kuwazuia kabisa watoto chini ya umri wa miaka 18 kuingia kwenye utumiaji wa bidhaa za tumbaku.

Mkakati huo ni pamoja na kufunga vifaa maalum vya kubaini moshi wa bidhaa za tumbaku kwenye majengo yanayotumiwa na watu wengi, kutenga maeneo maalum ya kuvutia sigara na kubandika jumbe za makatazo ya uvutaji wa sigara katika maeneo yaliyoanishwa, huku watakaokaidi wakitozwa faini ya kuanzia Sh. milioni 5 au kifungo kisichozidi miezi 12 au vyote na iwapo ni mtu binafasi atalipa faini isiyozidi Sh 200,000 au kifungo kisichozidi miezi sita au vyote.

Kaimu Meneja wa TMDA Kanda ya Ziwa Mashariki, **Bi. Sophia Mziray** alisema mkakati huo unaoanza mwaka 2020/21 hadi 2023/24 unalenga kupunguza matumizi na athari za kiafya zinazosababishwa na matumizi ya bidhaa za tumbaku, ambapo bidhaa hizo zinapaswa kutambulishwa kwa Mamlaka hiyo ifikapo Desemba 31, mwaka 2021 na maombi yote ya bidhaa mpya yataanza kupokelewa kuanzia Januari Mosi, mwaka 2022.

“Tunataka tuwakinge watoto chini ya miaka 18 na wasiotumia bidhaa hizo wasihamasike kutumia, kuwakinga wasiotumia bidhaa hizo na moshi unaotolewa na wavutaji, kuelimisha jamii juu ya madhara ya matumizi na kuhamasisha wavutaji kuacha kutumia na kuhakikisha bidhaa hizo zinaboreshwa,” alisema Mziray.

Alisisitiza kuwa kwa mujibu wa Sheria ya Tumbaku sura ya 121 bidhaa za tumbaku ni sigara, siga, sigarusi, misokoto, shisha, kiko na tumbaku ya unga, ambapo uvutaji wa sigara katika maeneo ya kutolea huduma za afya, maktaba, kuabudu, burudani, chakula, majengo ya ofisi, usafiri wa anga, maonesho na masoko umezuiwa.

Aprili 30, mwaka huu Waziri wa Afya, Maendeleo ya jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, **Dkt. Dorothy Gwajima** aliikaimisha TMDA jukumu la kusimamia na kudhibiti bidhaa za tumbaku na kuifanya Tanzania kuwa nchi ya pili Afrika ikitanguliwa na nchi ya Ghana kudhibiti bidhaa hizo, ambapo tayari Mamlaka hiyo imeanza kuchukua hatua kwa kuandaa mpango kazi.

Kwa mujibu wa takwimu za mwaka 2009 za Shirika la afya duniani zaidi ya watu bilioni 1.3 wanaotumia bidhaa za tumbaku wako katika nchi zinazoendelea ikiwemo Tanzania, ambapo zaidi ya watu Milioni 7 duniani wanakufa kila mwaka kutokana na magonjwa yatokanayo na matumizi ya bidhaa za tumbaku.

Katibu Tawala wa Wilaya ya Ilemela, **Bw. Said Kitinga** akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa mkoa wa Mwanza, **Mhandisi Robert Gabriel** ameagiza wananchi na Mamlaka katika mkoa huo kuanza utekelezaji wa kuweka jumbe za makatazo ya uvutaji sigara na shisha katika maeneo ya wazi huku akiiomba TMDA kujikita kutoa elimu kwa umma.

"Matumizi ya bidhaa za tumbaku yamekuwa yakiongezeka kila kukicha na madhara ya bidhaa hizi ni mzigo kwa serikali kwa sababu ya kugharimikia matibabu na kupoteza nguvu kazi kwa vifo. Nawasihi watendaji wa sekta ya afya ngazi ya Halmashauri na Mkoa washirikiane na TMDA kusimamia utekelezaji wa mpango huu na baada ya Desemba 31, mwaka huu ukaguzi uanze na hatua za kisheria zichukuliwe kwa watakaokaidi," alisema **Bw. Kitinga.**

Mratibu wa Udhibiti wa vifaa tiba wa TMDA, Kanda ya Ziwa Mashariki, **Bw. Mtani Njegere** alisema kuwa bidhaa za tumbaku zitahitaji kukidhi vigezo sahihi kuweza kupewa idhini ya kutumika nchini, ambapo Mamlaka itafanya kaguzi, ili kubaini iwapo kuna ukiukwaji wa taratibu katika utengenezaji wa bidhaa hizo.

Akielezea matumizi ya bidhaa hizo nchini alisema kuwa takwimu za Shirika la Afya Duniani (WHO) katika utafiti ulioitwa Global Youth Tobacco Surveys mwaka 2003 na 2008 katika mikoa ya Arusha, Dar es Salaam na Kilimanjaro ulionesha mwaka 2003 wanafunzi asilimia 18.1 (Arusha), asilimia 28.3 (Dar es Salaam) na asilimia 19.4 (Kilimanjaro) waliishi katika makazi ambayo wanafamilia wengine walikuwa wakivuta sigara.



Aliongeza kwa kusema kuwa mwaka 2008 wanafunzi asilimia 15.7 (Arusha), 19.4 (Dar es Salaam) na 17.6 (Kilimanjaro) waliishi makazi ambayo wengine walikuwa wavuta sigara huku 34.7 (Arusha), 39.4 (Dar es Salaam) na 32.3 (Kilimanjaro) walikuwa katika mazingira ya wavutaji sigara katika maeneo ya wazi.

Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Jiji la Mwanza, **Dkt. Pima Sebastian** amesema wataanza zoezi la kutoa elimu kwa wahusika wote katika maeneo yenye migahawa, hoteli, baa, majengo yanayotumika na watu wengi na maeneo ya wazi ili kuanza utekelezaji wa kuweka jumbe zenye makatazo, kutenga maeneo ya kutumia bidhaa hizo na kufunga vifaa vya kubaini moshi wa bidhaa za tumbaku kwenye majengo makubwa.

# SIMIYU YAJIPANGA KUDHIBITI MATUMIZI YA BIDHAA ZA TUMBAKU




*Katibu Tawala wa Mkoa wa Simiyu **Bi. Prisca Kayombo** akifungua kikao Kazi kati ya TMDA na Viongozi wa Mkoa, Halmashauri, Wafanyabiashara na Watendaji wa Sekta ya Afya wa Mkoa wa Simiyu juu ya udhibiti wa matumizi ya bidhaa za tumbaku mjini Bariadi mwezi Novemba, 2021. Katibu Tawala alimwakilisha Mkuu wa Mkoa wa Simiyu **Bw. David Kafulila.***

Mkuu wa Mkoa wa Simiyu, **Bw. David Kafulila** alisema kuwa mkoa huo uko tayari kuaanza udhibiti wa matumizi ya bidhaa za Tumbaku ili kulinda Afya ya jamii.

Akiongea kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa, Katibu Tawala wa Mkoa wa Simiyu, **Bi. Prisca Kayombo**, alisema wako tayari kusimamia utekelezaji wa shughuli za udhibiti wa matumizi ya bidhaa za tumbaku huku akiwaelekeza viongozi, wafanyabiashara na wananchi wa Mkoa wa Simiyu kuzingatia sheria, Kanuni na taratibu wakati wa utekelezaji wa jukumu hili.

“Maeneo yote ambayo bidhaa za tumbaku haziruhusiwi kutumika wekeni mabango kama sheria ilivyoelekeza. Wamiliki wa majengo wahakikishe uvutaji wa sigara unafanyika kwenye maeneo yaliyotengwa tu. Nawasihi tena wamiliki wa majengo yanayotumiwa na watu wengi, kuweka mabango kama sheria inavyoelekeza" alisema Kayombo.

Kwa upande wake Mganga Mkuu wa Mkoa wa Simiyu **Dkt. Boniface Marwa** alisema kuwa madhara ya matumizi ya bidhaa zitokanazo na tumbaku ni mengi ikiwemo saratani huku diwani kutoka kata ya Somanda **Bw. Robert Rweyo** akitoa ushauri

kwa Wizara ya Afya kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia kuanzisha mtaala kwa shule za msingi na sekondari juu ya madhara ya bidhaa za tumbaku ili kuwajengea watoto uelewa tangu wakiwa wadogo.

Naye Kaimu Meneja wa Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) Kanda ya Ziwa Mashariki, **Bi. Sophia Mziray**, alisema kwa mujibu wa tafiti kutoka shirika la afya duniani (WHO), magonjwa yanayosababishwa na matumizi ya bidhaa za Tumbaku ni kisababishi namba mbili cha vifo vyote vinavyotokea duniani huku idadi kubwa ya watu wanaotumia bidhaa hizo wakiwa kwenye nchi zinazoendelea.

Aliwaomba watendaji wa Sekta ya Afya ngazi ya Halmashauri na Mkoa kutoa kipaumbele kwenye suala la udhibiti wa matumizi ya bidhaa za tumbaku ili kuokoa maisha ya watanzania na kupunguza mzigo kwa Serikali kutokana na gharama kubwa zinazotumika kutibu magonjwa yanayosababishwa na matumizi ya bidhaa hizo.

"Kama nchi tulikuwa tunalitizama kwa mtazamo wa uzalishaji zaidi na hivyo kutoa hamasa kwa watu ili waweze kuzalisha bidhaa za tumbaku, lakini WHO katika tafiti zake imebainisha kuwa athari za kiafya zinazosababishwa na matumizi ya bidhaa hizi yanaongezeka kwa kasi kubwa sana" alisema Mziray.

"TMDA tumeshaandaa mpango kazi wa miaka mitatu (2021/2022-2023/2024) ambapo kwa mwaka wa kwanza tumejikita katika kutoa elimu zaidi kwani tunaamini wananchi wakielewa athari zinazosababishwa na matumizi ya bidhaa hizi, hawatumia hata wanaotumia wataacha na kutumia. Mkazo zaidi tumeweka katika kuwakinga watoto chini ya miaka 18 ili wasitumie kabisa na wasiotumia wasiathiriwe na moshi wa watumiaji. Nawaomba kila mmoja kwa nafasi yake tushirikiane katika kutoa elimu". aliongeza Mziray.

# TMDA YAWAASA WAFANYABIASHARA KUFUATA TARATIBU

Mamlaka ya dawa na vifaa tiba (TMDA) Kanda ya ziwa mashariki imesema inafanya kazi ya Kudhibiti ubora, usalama na ufanisi wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi kwa lengo la kulinda afya ya jamii.

Akizungumza na wafanyabiashara wa bidhaa za dawa, vifaa tiba na vitendanishi wakati wa semina ya siku moja jijini Mwanza, Kaimu Meneja wa Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) Kanda ya Ziwa Mashariki **Bi. Sophia Mziray** amesema kuwa bado kuna wafanyabiashara wachache ambao wamekuwa hawazingatia sheria na taratibu za kufanya biashara ya dawa, vifaa tiba na vitendanishi.

"Tumekuwa tukifanya ufuatiliaji wa mnyororo mzima wa usambazaji wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi baada ya kuingia nchini. Kupitia ufuatiliaji huu tumebaini uwepo wa wafanyabiashara wachache wanaofanya biashara bila kufuata sheria na taratibu za nchi kwa kuingiza na kuuza bidhaa zisizo na usajili nchini ambazo ubora, usalama na ufanisi wake haujathibitishwa na TMDA, hivyo kuhatarisha maisha ya watumiaji" alisema Bi. Mziray.

Ameongeza kuwa Kanda ya Ziwa Mashariki inasimamia shughuli za udhibiti katika Mikoa ya Mwanza, Mara, na Simiyu pamoja na mpaka wa Sirari, Uwanja wa Ndege wa Mwanza na mpaka wa Mwanza Kusini ambapo TMDA imeweka wakaguzi Kwenye maeneo yote ya mipaka na vituo vya forodha ili kuimarisha zaidi shughuli za udhibiti kwenye maeneo haya na kutoa msaada wa haraka kwa wafanyabiashara wanaoingiza na kutoa bidhaa hizi nchini.




*Kaimu Meneja wa Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) Kanda ya Ziwa Mashariki, **Bi. Sophia Mziray** akiwasilisha mada katika kikao na wafanya biashara wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi wa Mkoa wa Mwanza mwezi Novemba, 2021.*

Aidha amewaeleza wafanyabiashara kuwa Mamlaka itaendelea kufanya kaguzi mbali mbali katika maeneo ya kuuza, kuhifadhi na kutengeneza bidhaa zinazodhibitiwa na TMDA na hatua stahiki zitachukuliwa kwa watakao kiuka matakwa ya sheria.

***"Tuendelee kuwapa ushirikiano wakaguzi wanapofika kwenye maeneo yenu ya biashara maana huo ni wajibu wao na lengo la ukaguzi ni kulinda afya ya jamii kwa kuhakikisha kuwa dawa zinakuwa bora, zenye ufanisi na salama kwa matumizi ya binadamu"***